

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



BAJETI YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI 2019/2020.

Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, kwa kuzingatia taratibu zote, siku ya Alhamisi, tarehe 07 Februari ,2019 kwa kauli moja lilijadili na kuidhinisha bajeti yake ya **Tshs 125,174,373,000/=** kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo **Tshs. 84,958,373,000/=** ni Ruzuku kutoka Serikali kuu , **Tshs. 40,216,000,000/=** ni Fedha za makusanyo ya vyanzo vya ndani vya, Manispaa. Aidha kiasi cha **Tshs. 84,958,373,000/=** Fedha za ruzuku kutoka Serikali kuu, kinajumuisha kiasi cha **Tshs. 56,576,257,000/=** kwa ajili ya mishahara, kiasi cha **Tshs.2,493,774,000/=** matumizi mengineyo, **Tshs. 2,392,402,000/=** Fedha za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2019 na **Tshs.23,495,940,000/=** Fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kutoka Serikali kuu.

Mstahiki meya wa Manispaa ya Kinondoni Mh Benjamin Kawe Sitta amebainisha ,kuwa bajeti ya Mapato ya ndani imelenga kutatua changamoto zilizopo kwa kukuza uchumi na kupunguza umaskini ili kufikia maendeleo endelevu na imeongezeka kutoka **Tshs. 32,749,085,000/=** katika mwaka wa Fedha 2018/2018 hadi **Tshs 40,216,000,000 / =** katika mwaka wa Fedha 2019/2020 ,ongezeko la **Tshs. 7,466,915,000/=** kutokana na ubunifu wa vyanzo vipya vya mapato uliofanyika.


Alisema kuwa bajeti imeandaliwa kwa kuzingatia, sera na miongozo ya Kitaifa,sheria ya bajeti Na.11 ya mwaka 2015, Dira ya Taifa ya maendeleo 2025, Malengo ya millenia, mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini,(MKUKUTA),ilani ya CCM 2015-2020, sera ya Taifa ya Ukimwi, mipango shirikishi jamii ya fursa na vikwazo kwa maendeleo(O&OD) ya kata na Mitaa, sheria ya fedha ya serikali za Mitaa sura ya 290 iliyofanyiwa marekebisho mwaka, 2010,mpango wa maendeleo ya Taifa ya miaka mitano 2016/2017- 2020/2021 , Mpango wa maendeleo endelevu 2015-2030 na Mpango mkakati wa Manispaa ya Kinondoni wa 2016/2017- 2020/2021.

Aidha Mstahiki Meya aliyataja maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Bajeti kuwa ni, kuboresha na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Manispaa, kuboresha Miundombinu Afya, shule za Msingi na Sekondari, kuboresha miundombinu ya maji, barabara na kilimo mijini, kuimarisha kilimo mjini, kuboresha uhifadhi wa mazingira na ukusanyaji wa taka, kuboresha mazingira ya wafanyabiashara wadogowadogo, na kuimarisha ushirikishwaji wa jamii katika upangaji na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, na uwezeshaji wananchi kiuchumi kupitia mfuko wa wanawake na vijana kwa mfumo bora zaidi kupitia vyuo, taasisi na vituo vyetu.

Aidha, ili kufikia mafanikio hayo Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imedhamiria kusimamia kikamilifu mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusimamia mahusiano mazuri kati ya Serikali, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, na wadau wengine, kuendelea kujenga uwezo na ujuzi kwa watumishi katika utoaji wa huduma zilizo bora na haraka, kuimarisha utawala bora, uwajibikaji na uwazi, ikiwemo kujenga uwezo kwa viongozi wakiwemo waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa katika kusimamia shughuli za wananchi.

Mstahiki meya amewataka wananchi wa Kinondoni, kushirikiana na viongozi na Watendaji wa maeneo yao katika kutatua kero mbalimbali. Amesema kuwa anatambua uwepo wa changamoto nyingi ndani ya Manispaa ya Kinondoni ambazo haziwezi kutatuliwa zote ndani ya mwaka mmoja wa Fedha, hivyo, amewahakikishia kuwa changamoto zitaendelea kufanyiwa kazi kulingana na uwezo wa rasilimali zilizopo na kuwaomba wananchi kupitia Baraza la Madiwani kuwa na subira kwa kero zitakazosubiri bajeti ijayo. Aidha amewashukuru wote waliofanikisha bajeti hiyo zikiwemo kamati zote za kudumu za Manispaa, na hasa serikali kuu iliyoahidi kugharamia kiasi kikubwa cha fedha katika Miradi Mitatu ya Kimkakati ya ujenzi wa soko la Tandale, Soko la Magomeni na mradi Mkubwa wa kuboresha Fukwe za Cocobeach.

Imetolewa na:-



Sebastian M. Mhowera

**AFISA UHUSIANO WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONO**